**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

## KIKAO CHA TATU

**31 JANUARI, 2019**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

______________________

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

## KIKAO CHA TATU – TAREHE 31 JANUARI, 2019

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

Maelezo ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji kuhusu Muswada wa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira wa Mwaka 2018 *[The Water Supply and Sanitation Bill, 2018].*

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Muswada wa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira wa Mwaka 2018 *[The Water Supply and Sanitation Bill, 2018].*

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani juu ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kuhusu Muswada wa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira wa Mwaka 2018 *[The Water Supply and Sanitation Bill, 2018].*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:**

Maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali (Na. 4) wa Mwaka 2018 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 4) Bill, 2018].*

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA NA SHERIA:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali (Na. 4) wa Mwaka 2018 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 4) Bill, 2018].*

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani juu ya Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali (Na. 4) wa Mwaka 2018 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 4) Bill, 2018].*

## III. MASWALI:

**OFISI YA WAZIRI MKUU:**

**26. MHESHIMIWA CECILIA DANIEL PARESSO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Kwa kuwa tumebakiza mwaka mmoja kuelelekea Uchaguzi Mkuu, 2020; na ili Watanzania waliokidhi vigezo wapate haki ya kupiga kura, uboreshaji wa Daftari la Wapiga kura ni jambo lisiloepukika:-

Je, ni lini Serikali itaanzisha mchakato wa kuboresha Daftari la Wapiga kura.

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**27. MHESHIMIWA DANIEL EDWARD MTUKA (MANYONI MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Barabara ya Sulungayi inayoanzia Chikuyuni – Chibumagwa – Majiri – Ikasi (kilometa 76.2) ni barabara muhimu sana inayohudumia wakazi wa Bonde la Ufa katika Jimbo la Manyoni Mashariki kwa kusafirisha Chumvi, Samaki, Ufuta na Alizeti:-

Je, ni lini Serikai itaanza ujenzi wa barabara hiyo pamoja na daraja katika Mto Ngonjigwe.

## WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

**28. MHESHIMIWA CATHERINE VALENTINE MAGIGE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, ni lini Serikali itawalipa Wafanyakazi 545 wa KILTEX- Arusha ambao bado wanadai pensheni toka kiwanda hicho kilipofungwa

baada ya Mwajiri wao kutowasilisha michango yao kwenye Mfuko wa Jamii wa PPF.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**29. MHESHIMIWA RASHID ABDALLAH SHANGAZI (MLALO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kujenga Geti la kuingia Hifadhi ya Mkomazi katika Kijiji cha Kivingo.

**WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

**30. MHESHIMIWA OTHMAN OMAR HAJI (GANDO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:- Moja kati ya malengo makuu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ya Mwaka 2017/2018 ilikuwa ni kukamilisha kuandaa Sera mpya ya mambo ya nje:-

(a) Je, mpango huo umefikia wapi;

(b) Je, ni maeneo gani mapya kisera.

## WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

**31. MHESHIMIWA OSCAR RWEGASIRA MUKASA (BIHARAMULO MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:- Ni matarajio ya Wananchi wa Wilaya ya Biharamulo kwamba Serikali Kuu inao mpango mkakati ambao unazitambua fursa za viwanda, biashara na uwekezaji zilizopo Biharamulo.

Je, Serikali Kuu inasemaje kuhusu nafasi ya Wilaya ya Biharamulo kwenye ushiriki wa fursa za viwanda, biashara na uwekezaji ambazo zimeibuliwa na kutambuliwa na Serikali ili ziunganishwe na jitihada za Halmashauri ya Wilaya na Wananchi wenyewe.

## WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

**32. MHESHIMIWA MOSHI SELEMANI KAKOSO (MPANDA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:- Wilaya ya Tanganyika haina Mahakama ya Wilaya.

Je, ni lini Serikali itajenga Mahakama ya Wilaya sanjari na kuboresha Mahakama za Mwanzo.

**WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

**33. MHESHIMIWA ESTHER LUKAGO MIDIMU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Mradi wa maji toka Ziwa Victoria utapeleka maji kwenye Wilaya za Busega, Bariadi na Itilima kwa awamu ya kwanza:-

Je, kwa nini Serikali isipeleke maji hayo Makao Makuu ya Wilaya zote za Mkoa wa Simiyu katika awamu ya kwanza ili kutatua shida ya maji inayojitokeza mara kwa mara katika Miji hiyo.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**34. MHESHIMIWA ZAINAB ATHUMAN KATIMBA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, kuna utafiti wowote uliofanyika ili kubaini kama adhabu ya kuchapa Wanafunzi

inaongeza kiwango cha elimu na ufaulu katika Shule zetu nchini.

## WIZARA YA KILIMO:

**35. MHESHIMIWA JOSEPH MICHAEL MKUNDI (UKEREWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:- Mradi wa Kilimo cha Umwagiliaji wa Miyogwezi uliopo katika Kijiji cha Igongo Ukerewe ni tarajio kubwa la suluhu ya upungufu wa chakula; zaidi ya miaka mitano sasa tokea kufanyika uwekezaji wa zaidi ya shilingi milioni 700 bado mradi huo umetelekezwa:-

(a) Je, kwa nini Serikali imetelekeza mradi huo;

(b) Je, nini kauli ya Serikali kuhusu uendelezwaji wa mradi huo.

**36. MHESHIMIWA JOEL MWAKA MAKANYAGA (CHILONWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati Bwawa la Ikowa linalohudumia Skimu ya

umwagiliaji ya Chalinze iliyopo Kata ya Manchali na Bwawa la Buigiri iliyopo Kata ya Buigiri.

## IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

*(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na Kusomwa Mara ya Tatu)*

Muswada wa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira wa Mwaka 2018 *[The Water Supply and Sanitation Bill, 2018].*

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali (Na. 4) wa Mwaka 2018 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 4) Bill, 2018].*

**DODOMA** **S. KAGAIGAI**
**31 JANUARI, 2019** **KATIBU WA BUNGE**

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA